# KUMBUKUMBU ZA SHUGHULI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 21 OKTOBA 2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

| NA | JINA | WADHIFA/CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Dr. P. Henjewele | Mwenyekiti |
| 2. | V. Tigwela | Katibu |
| 3. | Mtundi Nyamhanga | Mjumbe |
| 4. | Fauzia T. Nombo | Mjumbe |
| 5. | H. Ugulum | Mjumbe |

**SEKRETARIATI.**

| NA | JINA | WADHIFA/CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Deodatus Mapunda | Katibu wa Kamati wa Manispaa |

**Agenda za Kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 21.10. 2021**

1. Kufungua Kikao.

2. Kupitia na kuidhinisha agenda.

3. Taarifa ya nyongeza ya Mpango wa Manunuzi pamoja na kuidhinisha orodha ya majina ya Wakandarasi watakaofanya kazi za Ujenzi katika mwaka 2021/2022.

4. Kufunga Kikao.

1/21. **Kufungua Kikao.**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe na kufungua Kikao saa 7.05 asubuhi.

2/21. **Kupitia na kuidhinisha agenda za Kikao.**

Wajumbe walipitia agenda zilizowasilishwa na kukubaliana kuwa zijadiliwe kama ifuatavyo:-

3/21. **Taarifa ya nyongeza ya Mpango wa Manunuzi pamoja na kuidhinisha orodha ya majina ya Wakandarasi watakaofanya kazi za Ujenzi katika mwaka 2021/2022.**

Iliwasilishwa Taarifa ya nyongeza ya Mpango wa Manunuzi pamoja na kuidhinisha orodha ya majina ya Wakandarasi watakaofanya kazi za Ujenzi katika mwaka 2021/2022. Ilielezwa kuwa inawasilishwa tarifa ya nyongeza ya Mpango wa Manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi katika Sekta ya elimu, Afya na Upangaji wa Machinga. Ilielezwa kuwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika Shule za Sekondari, chumba cha dharura (emergency unit) cha wagonjwa kama sehemu ya mapambano dhidi ya Uviko 19.

Aidha ilielezwa kuwa kwa kuwa manunuzi haya hayakuwepo kwenye Mpango wa Manunuzi, hivyo Kitengo cha Manunuzi kimeandaa nyongeza ya Mpango wa Manunuzi kwa mwaka 2021/2022 kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya mchakato wa manunuzi haujaanza kufanyika.

**Nyongeza ya Mpango wa Manunuzi.**

Nyongeza ya Mpango wa Manunuzi imeandaliwa kwa kuzingatia ongezeko la Miradi ambayo haikuwepo kwenye Mpango wa Manunuzi ulioandaliwa wa mwaka 2021/2022

ambao uliwasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni kupitia hati ya maazimio ya tarehe 15/7/2021.

Zaidi ya hayo ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa imepokea fedha kiasi cha Tshs. 3,220,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 146 na jengo la Afya la dharura.

Fedha hizi zitapokelewa nje ya Mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2021/2022 hivyo zitapelekea mabadiliko katika Mpango wa Manunuzi kwa kuongezeka kwa kiasi cha Tshs. 3,220,000,000.00 kwa shughuli za ujenzi.

**Ombi.**

Inaombwa idhini ili kiasi cha Tshs. 3,220,000,000.00 kipate idhini ya kufanya marekebisho kwenye Mpango wa Manunuzi.

**Azimio.**

Wajumbe waliridhia kiasi cha Tshs. 3,220,000,000.00 kipate idhini ya kufanya marekebisho kwenye Mpango wa Manunuzi kama ilivyowasilishwa.

**4/21. Idhini ya kuanza Mchakato wa Manunuzi ujenzi wa Madarasa na Chumba cha Dharura Hospitali ya Mabwepande.**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inakusudia kujenga madarasa mia na arobaini na sita (146) kwa shule za Sekondari na chumba cha dharura (emergency unit) katika Hospitali ya Mabwepande kwa gharama ya Tshs. 3,220,000,000.00. Manispaa ya Kinondoni katika mwaka wa fedha imepokea kiasi cha Tshs. 3,220,000,000.00 kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Ilielezwa kuwa tarehe 20 Oktoba, 2021, Menejimenti ya Manunuzi ilipokea dokezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa lililoandaliwa na Afisa Elimu Sekondari kwa ajili ya kuanza mchakato wa manunuzi wa ujenzi wa madarasa 122 katika shule za Sekondari ishirini na tano (25). Zabuni hii itakuwa ya wazi kwenda moja kwa Wakandarasi wenye sifa (eligibility), uwezo (ability) na uzoefu (experience), njia itakayotumika ni ya "single source" kwa mujibu wa kanuni Na. 161 na tangazo la Serikali Na. 333 la 2016.

**<u>Idhini ya kupitisha orodha ya Kandarasi, kablasha la Zabuni na majadiliano.</u>**

Menejimenti ya Manunuzi ya umma inaleta ombi kwa Bodi ya Zabuni kuidhinisha Wakandarasi wafuatao na kuidhinisha kablasha la zabuni na kufanyika majadiliano ya gharama, muda wa kuanza na kumaliza kazi, kijiridhisha na uwezo wan a uzoefu wa Mkandarasi. Wakandarasi hao ni Nepronic Building & Road Solution Co. Ltd, R&A works Co. Ltd. (Civil Works and Building Contractor), Works Contractors Limited, Ujenzi Store Limited, Nyagawa Investment, Muriran Contractor's Co. LTD, S.L.P 66652, Dar es salaam, Valosu Company Limited, P.O. BOX 10848, Dar es salaam, Basinda Construction, GC Ganda Classic Company Ltd (Civil $ Building Contractor), Macleseng Investment Co. Ltd (Civil works and Building Contractor), Sajo Civil Engineering $ building Construction Co.. Ltd, Mije Traders, Kanj International LTD, Jita Construction, Gecha Engineering Constructors (T) LTD, Rumuli Engineering $ Live Line technology, Jonus Constructors and Sky City Limited.

**Azimio.**
Wajumbe waliridhia Manispaa kuanza Mchakato wa Manunuzi ya ujenzi wa Madarasa na Chumba cha Dharura katika Hospitali ya Mabwepande.

**5/21.** **Kufunga Kikao.**
Menejimenti aliwashukuru Wajumbe wote na kufunga Kikao saa 7.27 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE** 5/11/2021